LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

# CHANGAMOTO ZA ELIMU KWA WATOTO WENYE ULEMAVU

Kwa Jamii Yenye Haki na Usawa

## WATOTO WENYE ULEMAVU NA ELIMU

***Changamoto na mapendekezo kwa watunga sera***

### Muhtasari

**Imebainika kuwa, mfumo wa elimu bado hauruhusu ufikiaji sawa kwa watoto wenye ulemavu kama watoto wengine. Katika tasnia ya elimu, changamoto zinazopatikana kwa Watoto hawa ni pamoja na; uhaba wa waalimu wenye uzoefu katika elimu kwa watu wenye mahitaji maalum, uhaba wa vifaa vya kujifunzia; kutokuwa na majengo ya shule rafiki kwa mfano ukosefu wa miteremko kwaajili ya viti vya magurugumu, mwanga wa kutosha kwenye madarasa, vyoo kwaajili ya watu wenye ulemavu, nafasi za kutosha kwaajili ya mizunguko ya vifaa na wasaidizi wao, pamoja na mitazamo au maoni hasi kutoka kwa watu wengine katika jamii na wenzao wa shule. Serikali inapaswa kuweka mfumo sahihi wa utekelezaji wa sera ili kuwezesha ufikiaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu.**

### Utangulizi

Watoto wenye ulemavu wana haki ya kufurahia haki ya kupata elimu kama watoto wengine. Tanzania pia imesaini na kuridhia maazimio tofauti ya kimataifa ambayo hutoa usawa katika elimu kama; Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Watu wenye Ulemavu, (2006) na Mkataba wa Haki za Mtoto, (1989). Pia mwaka 1994, Tanzania iliridhia Taarifa ya Salamanca juu ya elimu maalum ambayo ilisisitiza hitaji la kutoa elimu ya msingi kwa Watoto wenye mahitaji maalum.

Mnamo mwaka 2004 Tanzania ilitoa Sera ya Kitaifa ya huduma kwa watu wenye ulemavu, 2004 inayotoa wazi upatikanaji wa elimu ya msingi kwa watoto wote na wale wenye ulemavu watapewa kipaumbele na kutunga Sheria ya Watu wenye Ulemavu namba 9 ya mwaka 2010 ambayo inaainisha juu ya haki ya elimu kwa Watoto wenye ulemavu Pamoja na Mkakati wa Kitaifa wa elimu jumuishi mwaka 2017.

Licha ya kuwa na sera, sheria na mikakati mbalimbali inayojumuisha juhudi kubwa za serikali za kuongeza fursa kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu, bado watoto wengi wenye ulemavu hawapati haki hiyo ya elimu kama ipasavyo. Hivyo serikali bado inawajibu wa kutii makubaliano ya kimataifa iliyoridhia katika kufikia haki ya elimu.

**Baadhi ya sababu zinazuia upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu ni pamoja na:**

1. Bajeti finyu kushindwa kukidhi mahitaji ya kielimu kwa Watoto wenye ulemavu.

2. Utekelezaji duni wa sheria na sera zinazowahusu watu wenye ulemavu hususani katika masuala ya elimu kwa Watoto wenye ulemavu

> **Mpaka sasa kuna shule maalum 16 kwaajili ya watu wenye ulemavu na vitengo 159 vilivyo jumuishwa katika shule za kawaida nchi ni kote. Kuna vyuo vi wili vya Ualimu kwaaji li ya mafunzo maalum huko Tanga na Arusha Tanzania (LHRC, Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania, 2012) Lakini, uwepo wa shule hizi bado hauhakikishii**

Uhaba wa vifaa vya kujifunzia na ufikiwaji wa maeneo ya kujifunzia (umbali au majengo yasiyorafiki) na mitaala haijumuishi mahitaji ya walemavu. Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa serikali ya mwaka 2016/2017 ilionesha uhaba wa madarasa ya kusomea katika shule za msingi kuwa 85% na shule za sekondari kuwa 52% kwa mwaka 2017 vilevile utafiti wa Haki Elimu wa Aprili 2009 umebaini kuwa, 95% ya majengo ya shule hayazingatii mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu. LHRC, Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania, 2019 imeendelea kuonesha upungufu wa vyoo na madarasa katika sehemu mbalimbali za nchi hususani lake zone region ambapo pia ni sehemu zenye idadi kubwa ya watuwenye ulemavu.

**Hali ya majengo ya madarasa Tanzania**



Uhaba wa madarasa mwaka 2016/17
85% kwa shule za Msingi
52% kwa shule za sekondari

95% ya majengo hayazingatii mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu

3. Kukosekana kwa wataalam kama vile waalimu kwaajili ya watu wenye mahitaji maalum. LHRC, Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania, 2019 imeainisha kuwa Kigoma mpaka Mei, 2019 zaidi ya Watoto 3000 wenye ulemavu hawajaweza kufikia haki yao ya elimu kwa sababu ya ukosefu wa walimu wenye utaalamu katika elimu maalamu. Pia ripoti ya Uwezo iliyotolewa na Twaweza kwa mwaka 2019 imebainisha kuwa 13% tu ya waalimu walioshiriki katika utafiti huo wamefanyiwa mafunzo katika kufundisha watu wenye mahitaji maalum.

4. Tathmini duni na ukosefu wa takwimu sahihi za watoto na wanafunzi wenye ulemavu nchini. Hili linapunguza kasi ya mapambano dhidi ya ukosefu wa haki ya elimu kwa Watoto wenye ulemavu kwakua mipango mingi huzalishwa nje ya taarifa na takwimu sahihi na hivyo haijitoshelezi inapokuja kwenye utekelezaji

5. Udhaifu katika kusambaza na kutoa elimu na uhamasishaji juu ya sheria na sera zilizopo na kufanya watu wenye ulemavu kutokujua na kushindwa kudai haki zao na mara nyingi serikali huliachia jukumu hili asasi za kiraia pekee.

6. Ukosefu wa dhamira ya kisiasa ambapo wengi walio kwenye nafasi za maamuzi bado wanakosa kutoa kipaumbele kwenye masuala ya watu wenye ulemavu.

## MADHARA YAKE

Kukosekana kwa elimu kwa watoto wenye ulemavu husababisha kuongezeka kwa viwango vya kutojua kusoma na kuandika kati ya watu wenye ulemavu ambao baadaye hujikuta wakiwa katika nafasi za kutengwa kwani hawawezi kupata ajira au kujiendeleza kifedha. Hivyo kuunda sehemu ya familia masikini na pia wana uwezekano mkubwa wa kukuza watoto masikini.

Kuongezeka kwa umaskini katika familia au jamii hupunguza pato la kitaifa kwa nchi.

## NINI KIFANYIKE?

1. Sera ya kitaifa ya Mafunzo ya mwaka 2014 (National Education and Training Policy, 2014) inapaswa kupitiwa upya na kujumuisha ufafanuzi, aina na haki za mahitaji maalum.

2. Kuunda miongozo ya utekelezaji wa sera kuelezea jinsi mahitaji ya elimu kwa watoto walemavu yanapaswa kutolewa.

3. Kanuni ya 7 (b) ya Kanuni za Elimu (Kufukuza na Kutengwa kwa Wanafunzi kutoka Shule), 2002 (Regulation 7 (b) of the Education (Expulsion and Exclusion of Pupils from Schools) Regulations of 2002) zinapaswa kufafanuliwa ili kuepusha kuacha nafasi ya ubaguzi juu ya upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi walio na matatizo ya afya ya mwili au kiakili.

4. Serikali inapaswa kufanya kazi katika ushirikiano kati ya wizara mbalimbali, Asasi za kiraia, na taasisi za sekta binafsi zinazounga mkono haki ya kupata elimu.

5. Kuwezesha shule kwa kufadhili na kutenga rasilimali muhimu kwa kuendesha elimu ya mahitaji maalum.

6. Kubuni mitaala, njia za ufundishaji na tathmini zinazolingana na mahitaji tofauti ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

7. Kuongeza uwekezaji wake katika elimu ya watoto wenye ulemavu.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
**(MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
**S. L. P.** 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz Tovuti: www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
**S. L. P.** 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva,
Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
**S. L. P.** 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D,
**S.L.P** 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**@humanrightstz** **HakiTV**


**Kwa Jamii Yenye Haki na Usawa**